Maswali Tutakayouliza Ukituma Ombi la UNM Care au Out-of-County Care

Kila mtu anayetuma ombi la UNM Care au Out-of-County Care atapewa Mwakilishi wa Huduma za Kifedha wa kumsaidia kujaza ombi. Tafadhali tupigie simu ili kupanga miadi na Mwakilishi wako. Unapopiga simu, tujulishe iwapo ungependa kukutana naye ana kwa ana au kuwasiliana naye kwa simu.

Ili kupanga miadi yako, tafadhali piga simu kwa **505 272-2521 au 877 909-6661** (bila malipo) Jumatatu hadi Ijumaa kati ya saa mbili asubuhi (8:00 am) ana saa kumi na moja jioni (5:00 pm). Tuna Wawakilishi wanaozungumza Kihispania, Kivietinamu na Kinavajo. Ikiwa mmoja wao hapatikani kukusaidia, tutakuunganisha na mkalimani anayetoa huduma kwa njia ya simu au video.

Tunatoa huduma za ukalimani katika zaidi ya lugha 200, ikiwemo Lugha ya Ishara ya Marekani. Huduma za mkalimani ni za bila malipo. Tunatakiwa kisheria kutoa mkalimani kwa mtu yeyote anayemhitaji.

Taarifa hii itakusaidia kujiandaa kwa miadi yako na Mwakilishi wako wa Huduma za Kifedha. Inaorodhesha aina za maelezo na hati tutakazohitaji ili kukamilisha ombi lako la UNM Care au Out-of-County Care.

Tutauliza kukuhusu

Tutakuuliza maswali kukuhusu. Kwa mfano –

- Je, unaitwa nani?
- Je, anwani yako ni ipi? Nambari ya simu? Anwani ya barua pepe?
- Je, tarehe yako ya kuzaliwa ni ipi?
- Je, una bima ya afya? Ikiwa unayo, ni ya aina gani?

Tutauliza kuhusu ukubwa wa kaya

Kwa wagonjwa wenye umri wa miaka 18 na zaidi, “kaya” inajumuisha mgonjwa, mume/mke wake iwapo anaye na kila mtu ambaye mgonjwa anatarajia kudai kuwa mtegemezi katika maelezo ya kodi. Katika mipango hii miwili, mtu anayedaiwa kuwa mtegemezi katika maelezo ya kodi lazima awe anaishi nawe ili kuhesabiwa kama sehemu ya kaya yako.

Kwa wagonjwa wenye umri wa chini ya miaka 18, “kaya” inajumuisha mgonjwa, wazazi au walezi wake na kila mtu ambaye wazazi au walezi wake wanatarajia kudai kuwa ni mtegemezi katika maelezo ya kodi.

Ikiwa una maswali kuhusu wategemezi, tafadhali muulize Mwakilishi wa Huduma za Kifedha wakati wa mahojiano yako.

Tunaweza kuuliza maswali kama haya kuhusu watu wa kaya yako—

- Je, ni wanafamilia gani wanaishi katika kaya yako?
- Je, kila mtu ana umri gani?
- Je, kila mtu ana uhusiano gani na mgonjwa?
- Je, kila mtu ana aina ipi ya bima ya afya (ikiwa ipo)?

Tutakuuliza kuhusu mapato ya kaya yako

Tutakuuliza kuhusu kiasi cha pesa unachopata na kiasi ambacho kila mtu katika kaya yako hupata kila mwezi. Kiasi hicho kitatupatia mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya yako. Mapato ya **jumla** ni pesa unazopata **kabla ya** kodi zozote au makato mengine kukatwa. Kujua mapato yako ya jumla hutusaidia kuamua ikiwa unatimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care.

Tutauliza ikiwa unapata msaada kutoka kwa SNAP, TANF na/au WIC ya New Mexico. Ikiwa unapata msaada huo, tayari unatimiza sharti la mapato la UNM Care au Out-of-County Care.

Tutakuuliza kuhusu jinsi unavyopata pesa na kiasi cha pesa unachopata. Pia tutauliza ikiwa una bima na iwapo bima hutolewa kupitia kazi yako.

Tutauliza maswali hayohayo kuhusu kila mtu katika kaya yako. Tutauliza kuhusu aina nyingine za mapato ambayo wewe au watu wengine wa kaya yako huenda wanapata. Kwa mfano, fidia kutoka kwa mpango wa Social Security, fidia ya Kutokuwa na Ajira, fidia kwa Wanajeshi Wastaafu, fidia kwa Walemavu na fidia kutoka kwa Bureau of Indian Affairs.

Tutakuomba hati fulani za uthibitisho

Baada ya kujaza ombi lako pamoja, tutapitia **hati za uthibitisho** tunazotaka utoe. Tunaomba hati fulani za uthibitisho kwa sababu tunahitaji kuthibitisha wewe ni nani, mahali unakoishi, kiasi cha pesa unachopata na una pesa ngapi kwenye akaunti zako za benki na za uwekezaji. Maelezo haya yote hutusaidia kuamua ikiwa unatimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care.

Tafadhali hakikisha hutupatii hati halisi. Tunahitaji nakala tu.

Wewe ni Nani (Utambulisho)

Tutakuomba ulete 1 kati ya hati hizi kwa **kila mtu katika kaya yako**. Hati hizi hutusaidia kuthibitisha utambulisho wako na utambulisho wa kila mtu anayeishi nawe. Tutakubali yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa chini (nakala pekee tafadhali).

- Pasipoti (ya kigeni au ya Marekani)
- Cheti cha kuzaliwa (cha kigeni au cha Marekani)
- Kitambulisho cha picha (leseni ya dereva, kitambulisho kilichotolewa na serikali, kitambulisho cha kazi au cha shule)
- Kadi ya mpango wa Social Security
- Cheti cha Mzaliwa wa Kihindi
- Hati za talaka
- Rekodi za shule au rekodi za kituo cha kutunza watoto mchana
- Rekodi nyingine za serikali, kama vile viza (viza ambazo muda wake wa kutumika umeisha zinakubaliwa)
- Taarifa kutoka kwa mhudumu wa kesi, mhudumu wa afya ya jamii, mtoa huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua wewe na hali yako

Ikiwa huna yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapo juu, tujulishe. Tutashirikiana nawe kutafuta hati nyingine ili kutimiza sharti la uthibitisho wa utambulisho. Kumbuka, **huhitaji** kuwa na uraia wa Marekani au kuwa na hali fulani ya uhamiaji ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care.

Mahali Unakoishi (Anwani)

Tutakuomba ulete hati iliyo na jina na anwani yako. **Unahitaji moja tu kwa kaya nzima.** Tutakubali yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa chini (nakala pekee tafadhali).

- Waraka wa mshahara
- Bima ya gari
- Bili ya huduma ya nyumbani (umeme, gesi, maji, simu, intaneti)
- Mkataba wa kupangisha nyumba, hati ya rehani au hati ya ushuru wa jengo
- Bili au taarifa nyingine
- Uthibitisho wa kujiandikisha au kumwandikisha mtoto katika taasisi ya elimu

- Fomu za malipo ya kodi ya mapato
- Hati ya malipo ya Social Security, malipo ya ulemavu, malipo ya uzeeni au malipo ya kustaafu
- Taarifa kutoka kwa mhudumu wa kesi, mhudumu wa afya ya jamii, mtoa huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua na linalojua hali yako

Ikiwa huna yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa, tunaweza kushirikiana nawe ili kukubali hati tofauti.

Kiasi cha Pesa Unazopata (Mapato)

Ikiwa huna makazi, umefilisika au unapokea msaada wa SNAP, TANF au WIC, tunaweza kukuomba ulete hati zinazothibitisha hilo. Kwa mfano, barua kutoka kwa mhudumu wa kesi au shirika la jamii ambalo linajua hali yako; hati za mahakama; au barua kutoka kwa Idara ya Huduma za Kibinadamu.

Tutakuomba ulete hati zinazoonyesha kiasi cha pesa ambacho wewe na kila mtu katika kaya yako hupata kwa mwezi. Tutakubali yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa chini (nakala pekee tafadhali).

- Nyaraka za mshahara
- Fomu za malipo ya kodi ya mapato
- Barua kutoka kwa mwajiri inayotaja mapato yako ya kila mwezi
- Hati za kuweka pesa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki
- Barua au nakala za hundi kutoka kwa mipango ya Social Security, Worker’s Compensation, Veterans Affairs au Bureau of Indian Affairs.
- Rekodi za kumbukumbu za ajira ya binafsi
- Taarifa kutoka kwa mhudumu wa kesi, mhudumu wa afya ya jamii, mtoa huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua na linalojua hali yako

Ikiwa huna yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa, tunaweza kushirikiana nawe ili kukubali hati tofauti.

Ikiwa huwezi kuthibitisha mapato yako au hupati mapato, unaweza kuandika taarifa inayosema hivyo. Taarifa yako inapaswa kueleza jinsi unavyolipa gharama za kila siku kama vile chakula, nyumba na usafiri.

Kiasi Ulicho Nacho Katika Akaunti Zako za Benki na za Uwekezaji (Mali)

Tutakuomba ulete hati zinazothibitisha kiasi ulicho nacho katika akaunti zako za benki na za uwekezaji. Akaunti za uwekezaji zinaweza kuwa vitu kama hisa na dhamana au hazina za pamoja.

Ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care, huwezi kuwa na zaidi ya jumla ya $20,000 kwenye akaunti zako za benki (za kawaida na za kuweka akiba) na akaunti za uwekezaji.

Hatutakuomba uchukue pesa kutoka hazina yako ya kustaafu, dhamana, akaunti za kuhifadhi pesa bila kuzichukua kwa kipindi maalum (certificates of deposits, CD) ili kulipia bili zako za matibabu. Hata hivyo, ikiwa tayari umepokea pesa kutoka kwake katika mwaka huo au ikiwa fedha hizo zilifikia kipindi cha kutolewa katika mwaka huo (hii inamaanisha kuwa tarehe imefika ambapo lazima ulipwe kwa uwekezaji wako), fedha hizo zitahesabiwa kama mapato.

Tutakubali taarifa za akaunti za hivi karibuni za akaunti zozote za kawaida, za akiba na za uwekezaji ulizo nazo (nakala pekee tafadhali).

Kumbuka – Nyumba yako, gari na hazina ya kustaafu havijumuishwi. Huhitaji kuwasilisha hati zozote kuhusu mali hizo.

Tunaweza kukuuliza maswali mengine

Kwa mfano, ikiwa unahitaji huduma za matibabu kwa sababu ya ajali, tutaomba maelezo zaidi. Tunaweza kuuliza, ilikuwa ajali ya aina gani? Je, inalipiwa na mpango wa Fidia kwa Wafanyakazi? Je, unaweza kutuonyesha hati zozote zinazohusiana na ajali hiyo? Je, umewasiliana na wakili?

Hatimaye, tutakuuliza maswali haya mawili

1) Je, unaipa UNM Hospital ruhusa ya kuangalia taarifa za mapato yako na kuthibitisha ukubwa wa kaya yako (watu wanaoishi nawe) wakati wa kushughulikia ombi lako la UNM Care au Out-of-County Care?
2) Je, unaweza kuthibitisha kwamba maelezo uliyotoa katika mchakato wa ombi ni kweli na sahihi?

Tutataja kila swali kwa sauti na tutakuomba utaje jibu lako kwa sauti pia.